



**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Friday 6 May 2005 (morning)  
Vendredi 6 mai 2005 (matin)  
Viernes 6 de mayo de 2005 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Jibu suala moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi ya sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo ambaa umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nyngi.*

### **Tamthilia**

#### **1. Ama**

- (a) Kwa kiasi gani wahusika wakuu wawili wa kila kazi katika kazi mbili ulizozisoma katika sehemu hii wanatumiwa kuonyesha migogoro inayojadiliwa na waandishi?

*Au*

- (b) Onyesha vipi na kwa taathira gani vipengele vya “wakati” na “pahala” vimetumiwa katika tamthilia mbili ulizozisoma katika sehemu hii.

### **Riwaya**

#### **2. Ama**

- (a) Jadili huku ukionyesha jinsi mitiririko ya “ploti” ya riwaya mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii inavyoziathiri na kuzitofautisha riwaya hizo.

*Au*

- (b) Elezea jinsi waandishi wa riwaya mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii wanavyojishughulisha kwa upande mmoja, na matatizo ya wahusika binafsi, na kwa upande mwingine, wanavyoakisi matatizo ya jamii.

### **Ushairi**

#### **3. Ama**

- (a) “Katika ushairi mtu binafsi anajitokeza zaidi kuliko jamii.” Ijadili kauli hii kwa kutumia mashairi kadha uliyojitayarisha nayo katika sehemu hii.

*Au*

- (b) “Kipengele cha “urari wa kimuziki” ni muhimu sana katika sanaa ya ushairi.” Kwa kutumia mifano kadha ya mashairi uliyojitayarisha nayo, jadili vipi na kwa tofauti gani mshairi hukijenga kipengele hiki.

## Riwaya ya Mapenzi

### 4. *Ama*

- (a) “Hadithi ya mapenzi haikolei ila kwa mvutano baina ya wapenzi au wapenzi na maadui zao.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (b) “Wahusika katika riwaya ya mapenzi wanaweza kutoka nje ya mstari wa “uhalisia.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano mbalimbali kutokana na angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

## Masuala ya Ujumla

### 5. *Ama*

- (a) “Ingawa kazi ya fasihi huweza kufunza, kuonya na kuamsha, bado inabaki kazi ya sanaa kwanza kabla haijawa kitu kingine.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano katika kazi ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (b) “Mara moja mwandishi anajitenga na jamii anayoizungumzia na mara nyingine anajihusisha nayo na kuitetea.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutokana na kazi ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (c) “Kwa namna yoyote ile mwandishi hawezি kuepuka kuathiriwa na jamii yake katika uandishi wake.” Je, unakubaliana na kauli hii? Ijadili kwa kuitolea mifano kutokana na angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (d) “Sauti ya mwandishi husikika kwa namna mbalimbali katika kazi za fasihi.” Kwa kutumia kazi angalau mbili, elezea vipi na kwa namna ngapi sauti ya mwandishi hujitokeza katika kazi zao.